**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 23222761-5
*Fax No.* +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 941,
40490, Tambukareli,
**DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI ZA BUNGE

Vikao vya kamati za kudumu za Bunge vinatarajia kuanza siku ya Jumatatu tarehe 9 hadi 27 Machi, 2026 Bungeni Jijini Dodoma. Shughuli zitakazotekelezwa na Kamati za Kudumu za Bunge zinalenga kufanikisha maandalizi ya Mkutano wa Tatu wa Bunge la 13, ambao ni mahsusi kwa mjadala wa Bajeti ya Serikali uliopangwa kuanza siku ya Jumanne, tarehe 31 Machi, 2026.

Shughuli zitakazotekelezwa na Kamati katika kipindi hicho ni:-

(a) Waziri wa Fedha atawasilisha kwa Wabunge Mapendekezo ya Serikali ya Kiwango na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na Waziri wa Mipango na Uwekezaji atawasilisha kwa Wabunge Mapendekezo ya Serikali ya Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 katika Mkutano wa Wabunge wote, siku ya Jumatano tarehe 11 Machi 2026;

(b) Kamati 11 za Kisekta zitafanya ziara za kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(c) Kamati Kumi na Moja (11) za Kisekta na Kamati ya Bajeti zitachambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 za Wizara zote na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa mafungu (votes) yote ya Wizara za Serikali;

(d) Kamati ya Bajeti itachambua mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na Mapendekezo ya Kiwango na Ukomo kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(e) Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) zitafanya mafunzo ya uchambuzi wa taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kisha zitatembelea miradi iliyokaguliwa na CAG kwa lengo la kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwenye miradi hiyo;

(f) Vilevile, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) itafanya uchambuzi wa taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na kisha itafanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma; na

(g) Kamati ya Sheria Ndogo itafanya shughuli za uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa mezani wakati wa Mkutano wa Pili wa Bunge la 13.

Ratiba ya shughuli hizo za Kamati inapatikana katika tovuti ya Bunge ambayo ni www.bunge.go.tz

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
**DODOMA.**

05 Machi, 2026.